

Maswali

1. Mbona nduguze walimchukia Yusufu?
2. Yusufu aliota nini?
3. Yakobo alimtengenezea Yusufu nini?
4. Nduguze walimfanyia nini Yusufu?
5. Waishmaeli walikuwa wanaenda wapi?
6. Nani alijaribu kumuokoa Yusufu?
7. Nduguze walimpelekea Yakobo Nini?
8. Yakobo alifikiria kwamba nini alimuua Yusufu?
9. Yakobo alifanya nini aliposikia Yusufu amekufa?
10. Nani alinunua Yusufu kama mtumwa?

Majibu

1. Kwa sababu Yusufu alikuwa mwana mpendwa wa Yakobo
2. Yusufu aliota juu ya miganda ya nafaka, jua, mwezi, na nyota zikimwinamia
3. Yakobo alimtenezea Yusufu koti la rangi nyingi
4. Nduguze walimtupa ndani ya shimo na baadaye wakamuza kwa Waishmaeli
5. Waishmaeli walikuwa wanaenda Misri
6. Reubeni alitaka kumuokoa Yusufu
7. Nduguze walichukuwa koti lenye damu na kupelekea Yakobo
8. Yakobo alifikiria kwamba Yusufu alikuwa ameliwa na wanyama wakali
9. Alilia kwa muda mrefu
10. Potifa alinunua Yusufu kama mtumwa

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

11 Koti (vazi) la Yusufu

Marejeo

Mwanzo 37

Kiini cha somo

Kuonyesha vile wivu na chuki inawafanya watu kufanya mambo mabaya

Maneno maalum

- 1 Yusufu + Mwana mpendwa + Koti la rangi nyingi + Wivu wa nduguze
- 2 Ndoto + Miganda (vifurushi) ya nafaka + jua, mwezi na nyota + inama chini + kasirika
- 3 Lisha mifugo + Yusufu anaenda kuona nduguze
- 4 Nduguze wanataka kumuua + Reubeni akataa + Yusufu kwa shimo
- 5 Waishmaeli wakaja + Yusufu anauzwa + vipande 20 vya fedha + anaenda Misri
- 6 Reubeni anakasirika + damu kwa koti + Yakobo analia + Yusufu mtumwa Misri

11.1 Yusufu alikuwa mwana mpendwa wa Yakobo. Yakobo alimpenda zaidi kuliko wana wengine, na akamtengenezea koti lenye rangi nyingi. Nduguze walimchukia kwa sababu walimwonea wivu.

11.2 Yusufu alipotimia umri wa miaka kumi na saba, aliota ndoto na akaambia nduguze.

"Tulikuwa tukifunga miganda ya nafaka shambani, halafu mganda wangu ukasimama na zenu zikainamia yangu."

Nduguze walikasirika na wakamuuliza. "Tutakuinamia wewe?"

Yusufu aliota ndoto ingine tena na akawambia. "Jua, Mwezi na nyota kumi na moja ziliniinamia mimi." Nduguze walikaririka zaidi.

11.3 Wakati moja nduguze walienda kuchunga kondoo wa Yakobo huko shekemu. Baadaye Yakobo alituma Yusufu kwenda kuwajulia bali.

Alimwambia, "Enda uwaone ndugu zako, na uniletee habari yao." Yusufu alienda kuwatafuta na akawapata huko Dothani. Walipomuona na kabla awafikie, walipanga kumuua.

11.4 "Angalia," walisema, "Muota ndoto anakuja, tumuue, tumutupe kwa shimo na tuseme mnyama mkali amemuua."


"Hapana, mseimuue," Reubeni alisema, "mtupe ndani ya shima." Alitaka kumuokoa Yusufu baada ya nduguze kuondoka.

Yusufu alipowafikia, walimchukua na kurarua koti lake la rangi nyingi na wakamtupa shimoni.

11.5 Nduguze walikaa chini kukula waliona kundi la Waishmaeli wakija na ngamia zao, wamebeba viungo vya manukato wakipeleka Misri.

"Tuna faida gani tukimuua ndugu wetu?" Yuda akasema, "hebu tumuuze kwa Waishmaeli."

Walimtoa shimoni na kumuza kwa Waishmaeli kwa vipande ishirini yua fedha. Waishmaeli walimpeleka Misri.



11.6 Reubeni aliporudi na kumkosa Yusufu, alirarua nguo zake na kuwakasirikia ndugu zake.

Wakaua mwana mbuzi na kuchukuwa damu yake na kuweka kwa koti la Yusufu la rangi nyingi, Walipelekea Yakobo hilo koti.

"Tumepata hili koti shambani, ni la Yusufu?" Yakobo alilia mwanawe sana. "Ni koti la Yusufu," alilia, "mnyama mkali amemkula,"

Wanawe walijaribu kumtuliza lakini Yakobo hakutulia. "Nitaenda kaburini nikimlilia mwanangu," Yakobo alisema.

Lakini Yusufu alikuwa amepeleka Misri na kuuzwa kama mtumwa wa Potifa, mkuu wa askari wa Farao.